

## **UGONJWA WA GUMBORO (INFECTIOUS BURSAL DISEASE-IBD)**

### **Na Augustino Chengula**

Gumboro ni ugonjwa wenyе maambukizi makubwa unaowapata kuku wakionyesha dalili kuu kama viungo kuvimba, kuuma, kushindwa kufanya kazi, na kupungua kwa basa kadri muda unavyoendelea. Ugonjwa huu unawapata kuku wadogo wenyе umri kati ya wiki 3 hadi 6 ambaо basа yao inafanya kazi. Mara chache ugonjwa huu unaweza kuwapata kuku hadi wenyе umri wa wiki 18. Kwa marа ya kwanza ugonjwa ultambuliwa katika wilaya ya Delaware huko Marekani na ndiko ulikopewa jina hili la Gumboro. Baadaye kulingana na kuwa ugonjwa unashambulia kuku wenyе basа inayofanya kazi ukaitwa pia IBD. Tanzania ugonjwa huu ulithibitishwa miaka ya 1980 japo hisia zilikuwepo hata kabla ya hapо. Mashambulizi ya ugonjwa huu hulenga mfumo wa kinga ya mwili (basa) ya kuku na ndyo maana wadudu wengine wa magonjwa ambaо marа nyingi hawana madhara huanza kuonyesha madhara.

### **Kisababishi na ueneaji**

Ugonjwa wa Gumboro unasababishwa na kirusi aliye katika genera ya *birnavirus* ambaye anauwezo wa kukaa kwenye mazingira kwa muda wa angalau miezi 4. Kuku ndyo ndege pekee ambaye amekwisha ripotiwa kupata ugonjwa huu, huku aina zote za kuku wakiwa na uwezo wa kuupata ugonjwa huu. Kuku wadogo wasio na basа pamoja na wakubwa wenyе basа iliyosinyaa na kuifanya ipoteze uwezo wake wa kufanya kazi hawaupati ugonjwa huu.

Kuku wenyе maambukizi hudondosha virusi vya ugonjwa kuitia kinyesi kwenye mazingira. Maambukizi hutokea kutoka kwenye mabanda ya kuku yenye vijidudu vya ugonjwa, kinyesi toka kwa kuku wenyе maambukizi/ugonjwa, na chakula pamoja na maji yenye vijidudu vya ugonjwa. Maambukizi kwa kawaida huwa kati ya asilimia 0-20, lakini yanaweza fikia asilimia 60. Kuku waliopona ugonjwa huu na wale waliochanjwa wana uwezo wa kuusambaza ugonjwa kwa muda mrefu.

## **Dalili za Gumboro**

- Tangu maambukizi hadi kuanza kwa dalili huchukua muda mfupi wa siku 2-3
- Manyoya yasiyo na mvuto pamoja na kunyong'onyea kwa kuku (kutokuchangamka) ni dalili zinaashiria IBD japo zinaweza fananishwa na ugonjwa wa Coccidiosis.



Manyoya ya kuku yaliyokosa mvuto hasa maeneo ya kichwa na shingo, kuku huwa amenyong'onyea muda wote

- Uzito wa kuku hupungua kutokana na kukosa hamu ya kula
- Kuku hutetemeka
- Kuku huharisha mhalo wa maji maji na nyuma kwenye mkia huwa na mgandamano wa kinyesi



Kuku aliyeharisha na mhalo wake kugandamana maeneo ya nyuma chini ya manyoya yaliyokaribu na sehemu ya kutolea kinyesi

- Dalili inayoshitua ni vifo vya ghafla ndani ya muda mfupi na kisha kuku hupona na kurudi katika hali ya kawaida haraka. Kwa kawaida vifo huanza siku ya 3 tangu maambukizi na huongezeka kufikia vingi na kisha hupungua ndani ya siku 5-7.
- Kwa kawaida vifo vya kuku huwa kati ya asilimia 25 kuku wa nyama na 60 kuku wa mayai huku wa kienyeji wakiwa kati ya asilimia 20-30. Lakini vinaweza kufika asilimia 100 (kuku wote wakafa).
- Mara nyingi ugonjwa huu huwa na madhara makubwa unapojitokeza kwa mara ya kwanza, lakini huwa nafuu unapojitokeza kwa mara ya pili kwenye banda lenye kuku walewale.

#### **Dalili baada ya kuchinja kuku**

- Nyama yake huwa haina maji na imekonda
- Nyama za mapaja miguu ya nyuma na mabawa huwa nyeusi na zimejaa damu




- Nyama za mabawa na miguu ya nyuma zimevimba, zina rangi nyeusi na damu
- Figo huvimba (zimejaa damu) na ini pia inaweza kuvimba



Figo zilizojaa damu na kuvimba zikiwa na rangi nyeusi

-Ute mzito kwenye utumbo (mwembamba na mpana) huongezeka

**Busa:** Kuanzia siku ya 2 au 3 tangu maambukizi basa huanza kuvimba, hurudi kawaida na kisha husinyaa. Ikiwa imevimba huwa na rangi ya maziwa na ikisinyaa huwa na rangi ya kijivu. Wakati wote basa huwa na damu (vijitone na matone makubwa) na mara chache damu inaweza kusambaa basa yote. Damu inapoonekana imesambaa basa yote kuku huyo alipokuwa mzima alikuwa akitoa kinyesi kilichochanganyikana na damu.



Hatua ya mwanzo: Basa imejaa maji, imevimba ikiwa na utando wa rangi ya maziwa



Basa iliyopasuliwa ikionyesha madhara ndani yake ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa damu nyingi



Basa ikiwa imesinyaa. Kabla ya kusinyaa hupungua na kurudi kwenye hali yake ya kawaida, lakini huendelea kupungua zaidi.

### **Utambuzi**

- Mara nyingi utambuzi hufanywa kwa kutumia dalili kabla na baada ya kumchinja kuku
- Sampuli zinaweza kupelekwa maabara kwa utambuzi zaidi kwani ugonjwa huu hufanana na magonjwa mengine. Sampuli zinazoweza kuchukuliwa ni pamoja na kuku waliokufa muda mfupi, basa na spleen kwa ajili ya kuotesha virusi. Utambuzi pia unaweza kufanywa kwa kutumia njia za kiserolognia (chukua damu), histopathologia (chukua basa, bandama, figo utumbo na maini kwenye fomalini).

## **Magonjwa yanayofanana na Gumboro**

- Marek's disease
- Mycotoxicosis
- Coccidiosis
- Haemorrhagic syndrome
- Avian adenovirus infection
- Infectious bronchitis

## **Namna ya kupambana na Gumboro**

**Tiba:** Gumboro haina tiba (ugonjwa wa kirusi), kuuza kuku wote waliopona na kusafisha banda vizuri pamoja na kupuliza dawa ni njia inayopendekezwa na wataalamu. Kuto waruhusu kuku wenye ugonjwa kutembea ovyo pia ni njia inayosaidia kupunguza usambaaji wa ugonjwa.

**Kinga:** Uchangaji wa kuku ni njia muhimu ya kuzuia ugonjwa kwenye kuku na hasa wale kuku wa kuzalisha vifaranga. Ratiba ya uchangaji angalia [hapa](#)

## **MAREJEO**

1. Dr. Yonatan. Gumboro Disease, a Poultry Health and Management training course, Melbourne University, Australia.
2. OIE ***Terrestrial Manual*** 2008. **INFECTIOUS BURSAL DISEASE** (Gumboro disease), CHAPTER 2.3.12.
3. Christophe Cazaban, The control of Gumboro disease in chickens. *International Poultry Production — Volume 13 Number 4.*
4. Ivan Dinev, Infectious Bursal Disease (Gumboro) in:Diseases of poultry,

5. Preventive Veterinary Medicine - Infectious Bursal Disease/ Gumboro, Royal University of Bhutan.